Toleo 98 - Ramadhan 1446 H / Machi 2025 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Miaka Miwili Iliyopita Baada ya Tetemeko la Ardhi la Februari 6 Bado Mateso Hayana Mwisho

**HABARI NA MAONI**
Kutangaza Jamhuri nchini Syria ni Usaliti wa Mapinduzi ya Kiislamu!

**MATOLEO**
Trump na Mfuasi wako Netanyahu: Macho Yako Yamepofushwa

**JIBU LA SWALI**
Uhamishaji wa Watu wa Gaza



# Trump na Mfuasi wako Netanyahu: Macho Yako Yamepofushwa

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Afisi ya Habari Kitengo cha Wanawake

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 090/1446 Jumanne,19 Shaaban 1446 H 18/02/2025 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Miaka Miwili Iliyopita Baada ya Tetemeko la Ardhi la Februari 6 Bado Mateso Hayana Mwisho

Mnamo Februari 6, 2023, matetemeko makubwa mawili ya ardhi yenye kipimo cha 7.8 na 7.5, yaliyopiga kusini na katikati mwa Uturuki na kaskazini mwa Syria, yaliathiri mikoa 11 na kusababisha uharibifu mkubwa na kupoteza maisha. Takriban watu 54,000 nchini Uturuki na 8,500 nchini Syria walipoteza maisha katika matetemeko haya ya ardhi huku kitovu cha matetemeko hayo kikiwa Kahramanmaraş. Jumla ya waliopoteza maisha ilizidi 62,000, na mamilioni ya watu wakabaki bila makao. Hata hivyo, baadhi ya wataalamu wa huru na rasilimali za ndani zinaonyesha kuwa idadi halisi inaweza kuwa kubwa zaidi.

Baada ya matetemeko hayo makubwa ya ardhi, watu walilazimika kuishi katika mahema na nyumba za muda zilizotengenezwa kwa makontena ya chuma yaliyobadilishwa kuwa nyumba za makaazi. Katika kipindi cha miaka miwili iliyofuata, idadi ya watu wanaoishi katika miji ya makontena ilipungua kwa asilimia 7.78 pekee. Kulingana na takwimu za hivi punde zilizochapishwa na Idara ya Mawasiliano ya Afisi ya Rais mnamo Januari 2025, zaidi ya watu 650,000 bado wanaishi katika miji ya makontena.

Wakati huo huo, zaidi ya watu 300 waliripotiwa kutoweka baada ya tetemeko hilo la ardhi. Huku Waziri Ali Yerlikaya akizungumzia watu 75 waliopotea kufikia Novemba 2024, Naibu wa CHP wa Hatay, Nermin Yildirim Kara, anasema wana orodha ya watu 140 waliopotea, wakiwemo watoto 38. Wakati huo huo, familia zinalalamika kuhusu kutojali kwa serikali na wangali wanawasaka watoto wao.

Licha ya kuwa iko kwenye mojawapo ya njia zenye makosa makubwa zaidi duniani, uzembe na kutojali kwa serikali kulidhihirika wazi wakati wa tetemeko hilo, kwani ilishindwa kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya matetemeko ya ardhi, haswa katika miji mikubwa yenye msongamano mkubwa wa watu na ukuaji wa miji usio na mpango. Fauka ya hayo, ukosefu wa mpango madhubuti, mzuri na wa haraka wa utafutaji na uokoaji, pamoja na maandalizi duni ya timu na vifaa, ulifichua kiwango cha kutowajibika huku.

Tetemeko la ardhi la Marmara la 1999 lilifichua jinsi maamuzi ya serikali yalivyopuuzwa na mamlaka, huku taasisi zikifumbia macho na hongo kukithiri katika mashirika rasmi na ukaguzi wa majengo. Kushindwa huku kunatokana na Serikali kutokuwa na uwezo wa kuanzisha mifumo ya udhibiti. Kwa kweli, moto wa hoteli huko Bolu mnamo 21 Januari 2025 pia unachukuliwa kuwa matokeo ya moja kwa moja ya kushindwa huku. Moto wa 21 Januari 2025 katika hoteli ya Bolu ni matokeo ya moja kwa moja ya haya: uzembe, ukosefu wa ukaguzi, na ulafi wa kirasilimali - kuanzia mmiliki wa hoteli, idara ya zima moto iliyotoa ripoti ya moto, manispaa iliyotoa cheti cha usalama wa moto, jimbo na Wizara ya Utalii ambao wote waliidhinisha bila udhibiti - na kugharimu maisha ya watu 78. Walakini, kila mmoja anamtupie mwengine lawama, na hakuna anayechukua jukumu. Hatimaye, uhalifu na sababu zake ni dhahiri. Ni ulafi wa mabepari na watawala wanaowatumikia, wakiamini maisha haya kamwe hayatakwisha na lengo lake pekee ni kujilimbikizia mali.

Uongozi wa Kiislamu, unaotafuta tu radhi za Mwenyezi Mungu na Pepo ya Milele kama lengo pekee la maisha, huhakikisha bila kuchoka usalama wa maisha, mali, na heshima ya watu wake. Hakuna uwekezaji uliomkubwa sana; daima unajitahidi kupata uboreshaji, ukilenga kusimamisha mfumo wa Mwenyezi Mungu wa uadilifu, usalama, na ustawi katika nyanja zote za maisha – daima kwa njia bora zaidi inavyoweza, kwani lengo lake kuu ni radhi za Mwenyezi Mungu (swt).

[وَأَحۡسِنُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلۡمُحۡسِنِينَ]

"Na fanyeni wema. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema." [Al-Baqarah 195]

**Kitengo cha Wanawake**

**katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Kutangaza Jamhuri nchini Syria ni Usaliti wa Mapinduzi ya Kiislamu!

**Habari:**

Ahmed al-Shara, ambaye alifanya ziara yake ya kwanza ya kigeni nchini Saudi Arabia baada ya kuchukua kiti cha Urais nchini Syria, alitoa taarifa muhimu kuhusu mustakabali wa Syria sambamba na ramani ya utendakazi ya kisiasa ambayo amedumisha katika mahojiano na televisheni ya Syria. Akiahidi kukuuza uchumi wa soko huru na vifaa vya uwekezaji, Shara alisema, "Syria ni nchi ambayo itahifadhi hali yake ya asili, muundo wa serikali utakuwa wa jamhuri, kutakuwa na bunge, tawi la utendaji na mamlaka zinazofanya kazi kwa ushirikiano kati yao." alitumia maneno yake. (Mawakala)

**Maoni:**

Ahmad al-Shara amewavunja moyo watu wa Syria na mujahidina wa dhati kwa kauli zake baada ya operesheni ya kijeshi iliyoanzishwa baada ya watu wa Idlib kuendelea kudai kufunguliwa tena kwa mipaka kwa miaka mingi na ambayo ilisababisha dhalimu Bashar al-Assad kutorokea Urusi mnamo 8 Disemba 2024. Zinaendelea pia kuwafurahisha makafiri wa Magharibi, haswa Marekani na washirika wao wa ndani katika kanda hii.

Shara ambaye alitoa msamaha kwa mabaki ya utawala huo mara tu alipochukua madaraka na kuwalingania wananchi kwenye amani na maridhiano kwa kusema kuwa hawatatenda kwa hisia za kulipiza kisasi, anajaribu kila njia kuhakikisha jina la mapinduzi ya Syria halinasibishwi na Uislamu. Kila Muislamu anayefuata siasa zake kwa akili anaona kwamba anajifanya kana kwamba anawajibika kwa Magharibi na mfumo wa kimataifa, na sio kwa watu wa Syria. Subhanallah!

Ahmad al-Shara hataji maamrisho na masuluhisho ya Uislamu katika hotuba yake yoyote, kana kwamba anauonea aibu Uislamu. Anazungumza kana kwamba itikadi na utaratibu wa Uislamu hauna uwezo wa kuwaunganisha watu wa Syria na kutawala kwa uadilifu, kana kwamba dini ya Mwenyezi Mungu haitoi ruwaza ya maendeleo. Akiongea hivi, anajidhalilisha yeye mwenyewe na mapinduzi ya Syria. Haijalishi ni maelezo gani yanaangaliwa, kuna makubaliano na kujisalimisha! Inamaanisha nini kutaka amani na umbile la Kiyahudi wakati liliposhambulia Syria, kuharibu nguvu zake zote za kijeshi, kupanua ukaliaji wake wa kimabavu wa Milima ya Golan? Watu wa Syria wamepiga kelele kwamba wanataka sharia na Khilafah kwa muda wa miaka 13, wamelipia gharama kubwa kwa hili, huku mujahidina kutoka pande zote za dunia walipigana kwenye njia hii, unamaanisha nini kusema "Syria itakuwa Jamhuri ya Kiarabu"?

Ina maanisha nini kuitelekeza bendera ya Tawhid na kuchukua bendera ya Sykes-Picot? Ina maanisha nini kumpongeza rais mwenye kiburi wa Marekani, kafiri mkoloni, adui mkubwa wa Uislamu na Waislamu, anayezifungamanisha Urusi na Iran, waungaji mkono wakubwa wa Bashar al-Assad, juu ya watu wa Syria, ambaye aliipa Uturuki nafasi ya kuyapotoa njia mapinduzi, na kusema kwamba anaamini kwamba ataleta amani na utulivu Mashariki ya Kati? Inamaanisha nini mara kwa mara kutumia misemo kama vile "serikali jumuishi" na "serikali ya kiraia" kuashiria na kutoa ahadi kwa vyombo vya habari vya Magharibi kwamba wanakumbatia demokrasia? Uislamu uko wapi katika hili? Izza iko wapi katika hili? Mtazamo wa kisiasa uko wapi katika hili? Je, kauli zote hizi eti zilitolewa kwa ajili ya Syria kuinuka kweli zitawaridhisha makafiri wa Magharibi? Hapana! Kwa sababu Mwenyezi Mungu ameamrisha waziwazi:

**[وَلَن تَرْضَى عَنكَ الْيَهُودُ وَلاَ النَّصَارَى حَتَّى تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ]**

"Mayahudi hawawi radhi nawe, wala Wakristo, mpaka ufuate mila yao..." (Baqarah 120)

Kila makubaliano yatakayofanywa yatapelekea kwenye makubaliano mengine. Pindi haramu ikisha fanywa, haramu nyingine itakuja kwa urahisi moyoni. Shetani atanong'ona kwamba hakuna njia nyingine isipokuwa kuingiliana na makafiri, akisema "dhurufu zinalazimisha jambo hilo. Ugaidi"; lakini mwishowe, makafiri hawa watawalizimisha Waislamu kuwaelekezea bunduki ndugu zao kwa badali ya uungaji mkono wao. Ukweli ni, kuuliwa kwa mujahidina nchini Syria kunaonyesha dhahiri hali hii. Mauaji haya yataelekezwa kwa wale wanaopinga Syria kuwa jamhuri ya kisekula ya Kiarabu chini ya kisingizio cha "kupambana na ugaidi"; wale ambao hawaridhiki na amani na Mayahudi, wale ambao wanawakumbusha wasimamizi wa mapinduzi na kutaka kusimamishwa kwa Khilafah ya Kiislamu nchini Syria. Ahmad al-Shara alisema, "Tumetupa vumbi la udhalilifu na unyonge juu ya Damascus." Kwa maneno yake hayatabadilisha ukweli huu. Hakuna ushahidi unaotangaza kwamba mapambano ya Kiislamu baada ya madikteta kupinduliwa. Hata hivyo, kuna uthibitisho imara kwamba kuegemea kwa makafiri, kuingia katika miundo yao ya kifikra na kisiasa, na kuwafanya marafiki makafiri badala ya waumini kutawatia hasara duniani na kesho akhera!

**[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَخُونُواْ اللّهَ وَالرَّسُولَ وَتَخُونُواْ أَمَانَاتِكُمْ وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ]**

"Enyi mlio amini! Msimfanyie khiana Mwenyezi Mungu na Mtume, wala msikhini amana zenu, nanyi mnajua. " (Anfal 27)

Namuomba Mwenyezi Mungu (swt) awape nguvu na busara watu wa Damascus na mujahidina wenye ikhlasi kuyalinda mapinduzi ya Syria dhidi ya khiyana na mitego, na awasaidie Waislamu wote kuendesha Sharia.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**
**Muhammad Emin Yildirim**

# Trump na Mfuasi wako Netanyahu: Macho Yako Yamepofushwa

Trump na wapambe wake wanaendelea kurudia madai yao kwamba atainunua Gaza na kuimiliki.

[كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ إِنْ يَقُولُونَ إِلَّا كَذِباً]

“Ni neno kuu hilo litokalo vinywani mwao. Hawasemi ila uwongo tu.” [Surat Al-Kahf:5]

“Mapema leo, Rais Trump wa Marekani alithibitisha mpango wake wa Marekani kuchukua udhibiti wa Gaza na kuwafukuza Wapalestina, akisema kwamba amejitolea kuinunua na kuimiliki Gaza. Kauli hii ilitolewa na Trump mnamo Jumapili jioni ndani ya ndege ya Air Force One alipokuwa akielekea New Orleans kuhudhuria Super Bowl." (BBC, 10/2/2025) Baadaye, wakati wa mkutano wake na Mfalme wa Jordan, alisema: "Wapalestina wataishi kwa usalama mahali pengine, nje ya Gaza, na ninaelewa kwamba tuna uwezo wa kufikia suluhisho," kulingana na maneno yake. Trump aliongeza, "Tutaisimamia Gaza vizuri sana, lakini hatutainunua," kama ilivyoripotiwa na Reuters. Alipoulizwa kuhusu 'Israel' kunyakua Ukingo wa Magharibi, Trump alisema, "Itafanya kazi," kulingana na taarifa yake. (Reuters - Erem News, 11/2/2025) Hapo awali, alikuwa amesema kwamba "'Israel' itaikabidhi Gaza kwa Marekani baada ya mapigano kumalizika," akitarajia Marekani kuwa na "umiliki wa muda mrefu" wa eneo la Palestina. (Al Jazeera, 6/2/2025)

Dhalimu huyu, aliyepagawishwa na kiburi chake mwenyewe, haelewi anachokisema. Anafikiri kwamba Gaza ni milki yake au ya mwanachini wake, Netanyahu, inayoweza kununuliwa, kuuzwa, au kukabidhiwa! Kiburi chake kimemtia upofu na kumnyima busara. Amesahau au amechagua kupuuza hatima ya wale waliokuja kabla yake.Alitanguliwa katika udhalimu wake na wafalme wa Fursi na Rumi. Khosrow alipopata habari za ujio wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), kiburi chake kilimtawala, hivyo akamtuma mmoja wa watumishi wake kumwambia: Nenda Bara Arabu ukaniletee kichwa chake.” Haya ndiyo aliyoyasema kutokana na upotovu wake! (Ibn Hisham amesema katika Serah yake: Khosrow alimwandikiwa Badhan: “Imenifikia habari kwamba mtu miongoni mwa Maquraysh amezuka mjini Makka, anadai kuwa ni Nabii. Nenda kwake na umfanye ajisalimishe. Ikiwa atattubu, muwacha; vyenginevyo, nitumie kichwa chake.” Hatima yake ilikuwa kuanguka kwa ufalme wake, na utawala wa Khosrow ukasalia kuwa kumbukumbu tu chini ya mashambulizi ya jeshi la Waislamu. Fursi hatimaye ikakombolewa, na nuru ya Uislamu ikaangaza ndani yake. Ama mfalme wa Rumi, alikusanya jeshi ili kuwamaliza Waislamu katika eneo la Yarmouk, lakini hatima yake ilikuwa kushindwa. Akakimbia Sham, akiiambia: “Kwaheri, ewe Sham, kwa kwaheri isiyo na kurudi tena!” Aliondoka kwenda mahali alipozaliwa, Konstantinopoli, mpaka ilipotekwa na kuwa nchi ya Uislamu. Ama kuhusu Mfalme wa Kirumi, alitayarisha jeshi la kuwaangamiza Waislamu huko Yarmouk, lakini mwisho wake ulikuwa kushindwa kabisa. Alikimbia Sham, akisema, * "Kwaheri, Sham, kwaheri isiyo na kurudi tena," * akirudi kwenye eneo lake la kuzaliwa huko Konstantinopoli - hadi hapo, pia, ilipotekwa na kuwa sehemu ya ardhi ya Uislamu.

Ama Mayahudi wanabaki kuwa duni, wamedhalilishwa popote waendako.

[ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ أَيْنَ مَا ثُقِفُوا إِلَّا بِحَبْلٍ مِنَ اللهِ وَحَبْلٍ مِنَ النَّاسِ وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِنَ اللهِ وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الْمَسْكَنَةُ]

“Wamepigwa na udhalili popote wanapo kutikana, isipo kuwa wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu. Na wakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na wamepigwa na unyonge.” [Surat Aal-i-Imran:112]. Walikata fungamano lao na Mwenyezi Mungu kwa kuwaasi Mitume Wake, na tegemeo lao pekee lililobaki ni juu ya msaada wa watu—msaada ambao bila shaka utakatiliwa mbali na Amri ya Mwenyezi Mungu, kwa wakati uliopangwa, kwa mikono ya wanajeshi wa Uislamu, wakiongozwa na Imam wao. Watapigana nyuma yake na watalindwa kwaye, kama Mtume (saw) alivyosema:

«إِنَّمَا الْإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ»

“Kamanda (wa Waislamu) ni ngao kwao. Wanapigana nyuma yake na wanalindwa na (yeye kutokana na madhalimu na wavamizi).”

Enyi Waislamu…Trump na mfuasi wake Netanyahu wanasahau historia ya watu wao na fedheha yao ya zamani mbele ya ulimwengu. Wanasahau udhalilifu wao na utukufu wa Uislamu juu yao wakati Khilafah ilipoasisiwa. Katika siku hizo, sio mababu wa Trump wala Netanyahu wangesubutu kusema hata neno moja kuhusu kununua hata shubiri moja ya ardhi ya Kiislamu, achilia mbali Gaza, ardhi ya Hashim. Badala yake, wangeinamisha vichwa vyao kwa kutajwa tu futi moja ya ardhi ya Kiislamu.

Ndio, wanawaona Waislamu leo bila Khilafah kwa zaidi ya miaka mia moja. Wanaona ardhi za Waislamu zikiwa zimegawanyika, zikitawaliwa na mawakala wao—watawala vibaraka wanaowatumikia. Hivyo, Trump anatangaza wazi mpango wake wa kuwafukuza watu wa Gaza, kuinunua na kuimiliki. Wakati huo huo, watawala wa ardhi za Waislamu hawafanyi lolote kuyakusanya majeshi yao kuikomboa Gaza na kumshambulia Trump na mfuasi wake kwenye nyuso zao. Badala yake, Trump anasema kwa ujasiri kwamba watawala hawa hatimaye watakubaliana na mpango wa uhamishaji na kila kitu anachotaka. Alipoulizwa kwa nini viongozi hao wanadai hadharani kukataa mpango huo, alijibu: "Watakubali. Wanasubiri tu kukutana nami." Anatamka hili waziwazi, lakini bado wangali wanakimbilia kukutana naye bila aibu!

Enyi Waislamu…Khilafah itaregea, na kuhitimisha utawala wa vibaraka hawa wa fedheha katika ardhi za Waislamu. Itaregea, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, hii

***Endelea... UK 5***

ni yakini, kwa sababu Mwenyezi Mungu ameahidi:

[وَعَدَ اللهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا
اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ]

“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao” [Surat An-Nur:55].

Mtume (saw) pia alitabiri kuregea kwa Khilafah baada ya kipindi hiki cha utawala dhalimu:

«ثُمَّ تَكُونُ مُلْكاً جَبْرِيَّةً فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللهُ أَنْ تَكُونَ، ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ
يَرْفَعَهَا، ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ. ثُمَّ سَكَتَ...»

“Kisha kutakuwa na kipindi cha utawala wa kidhalimu, ambao utadumu kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyo. Kisha atauondoa apendapo kuuondoa. Kisha itakuwepo Khilafah na kwa njia ya Utume.” (Ahmad)

Hata hivyo, kama tunavyosema mara kwa mara, na kama watu wenye hekima wanavyoelewa, amri ya Mwenyezi Mungu ni kwamba Malaika hawatashuka kutoka mbinguni ili kutusimamishia Khilafah tukiwa tumekaa bila kufanya kazi. Bali nusra yake na bishara zake zinawajia walio muamini, na kuwazidishia uongofu, na kuwaweka imara katika vita, mpaka awape ushindi:

[نَصْرٌ مِنَ اللهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ]

“nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi ulio karibu! Na wabashirieni Waumini!” [Surat As-Saff:13].

Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, kwa kuwa dalili zinazoashiria kuregea kwa Khilafah zinaonyesha ukaribu wake. Ummah wa Kiislamu ni Ummah hai, changamfu, unaosonga mbele kwa shauku kuelekea kusimamisha Khilafah na kuunga mkono juhudi hii mpaka itimie ahadi ya Mwenyezi Mungu. Baada ya hapo, utaungana kuilinda na kushikamana nayo… Hakika Umma unaregea kwa haraka kwenye njia yake ya asili, ambayo kwayo Mwenyezi Mungu aliiuleta. Kama Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyosema:

[كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ
بِاللهِ]

“Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu.”[Surat Aal-i-Imran:110].

Ndani ya Ummah huu, kuna kundi lenye ikhlasi lililojitolea kwa Mwenyezi Mungu, lenye uaminifu kwa Mtume Wake (saw). Wanasonga mbele, mchana na usiku, mpaka itimie ahadi ya Mwenyezi Mungu na bishara njema ya Mtume mikononi mwao. Hawaogopi kulaumiwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na azma yao haitayumba kwa idhini yake mpaka itimie amri yake. Ni kama Mtume (saw) alivyosema katika hadith iliyopokewa na Muslim:

«لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي ظَاهِرِينَ عَلَى الْحَقّ لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَذَلَهُمْ حَتَّى يَأْتِيَ أَمْرُ
اللهِ وَهُمْ كَذَلِكَ...»

“Kundi la watu kutoka kwa Umma wangu daima watabaki kuwa ni wenye kudhihirisha haki. Anayejitenga nao hataweza kuwadhuru. Watabaki katika njia hii mpaka amri ya Mwenyezi Mungu ije na ilhali wako katika njia hii.”

Hivyo, Khilafah itaregea, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, kupitia juhudi za watu wake baada ya kipindi hiki cha utawala dhalimu. Kisha, umbile la Kiyahudi litatokomezwa, na Palestina itaregeshwa kikamilifu kama sehemu ya ardhi ya Uislamu. Muslim pia anasimulia kutoka kwa Abu Huraira kwamba Mtume (saw) amesema:

«لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى يُقَاتِلَ الْمُسْلِمُونَ الْيَهُودَ فَيَقْتُلُهُمْ الْمُسْلِمُونَ..»

“Kiyama hakitasimama mpaka Waislamu wapigane na Mayahudi, na Waislamu watawaua...” Fauka ya hayo, hata Rumi itakombolewa na mikono ya Waislamu, kama vile Constantinople ilivyokombolewa. Ahmad amepokea kwamba Abdullah bin Amr bin al-As amesema: “Tulipokuwa tukiandika karibu na Mtume wa Mwenyezi Mungu (ﷺ), mtu mmoja alimuuliza: ‘Ni upi kati ya miji miwili itakaokombolewa kwanza, Konstantinopoli au Roma?’ Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akajibu:

«مَدِينَةُ هِرَقْلَ تُفْتَحُ أَوَّلاً يَعْنِي قُسْطَنْطِينِيَّةَ»

“Mji wa Heraclius utakombolewa kwanza, ikimaanisha Konstantinopoli.”

Enyi Waislamu…Ni miongoni mwa fedheha kubwa zaidi kwamba dola katika ardhi za Uislamu zinalizunguka umbile la Kiyahudi mithili ya bangili kwenye kifundo cha mkono, na bado hazikusanyi majeshi yao kupigana na kuitakasa ardhi iliyobarikiwa kutokana na uchafu wake. Ni miongoni mwa fedheha kubwa zaidi kwamba Trump anatangaza waziwazi kuwahamisha watu wa Gaza bila ya kujali watawala wa Waislamu wanaoizunguka. Na alipoulizwa kuhusu viongozi wa Kiarabu na Waislamu kukataa kuhamishwa kwa watu wa Gaza, anajibu kwa kujiamini kwamba hatimaye watakubali, hivyo kuwadhalilisha, lakini hawaoni haya. Ni miongoni mwa fedheha kubwa kwamba hawasubutu hata kuisusia Marekani au kukataa kukutana na Trump, licha ya kauli zake kuwafichua. Badala yake, wanampongeza, na anapowaita, wanakubali, wanamtembelea na kusikiliza kwa unyenyekevu.

Ni miongoni mwa fedheha kubwa kwamba majeshi ya Waislamu yanabaki yametulia tuli huku yakishuhudia uvamizi katili wa Kiyahudi, maangamivu ya maisha ya watu, miti na mawe, wakijidanganya nafsi zao kwamba utiifu kwa watawala wao kwa kujiepusha na kupigana na Wayahudi utawaokoa. Badala yake,

[يُرِيهِمُ اللهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ]

“Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyo waonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao.” [Surat Al-Baqara:167] na watasema wakati wakati majuto hayatawanufaisha kitu!

[إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ]

“Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia.” [Surat Qaf:37]

**H. 14 Sha'aban 1446**
**M. : Alhamisi, 13 Februari 2025**

**Hizb-ut-Tahrir**

# JIBU LA SWALI

# Uhamishaji wa Watu wa Gaza

**Swali:**
Al Jazeera ilichapisha kwenye tovuti yake mnamo tarehe 26/1/2025: “Rais wa Marekani Donald Trump alisema kwamba anaishinikiza Jordan, Misri na nchi nyingine za Kiarabu kupokea wakimbizi zaidi wa Kipalestina kutoka Gaza, baada ya vita vya Israel dhidi ya Ukanda huo kusababisha mgogoro wa kibinadamu. Alipoulizwa ikiwa hili lilikuwa pendekezo la muda au la muda mrefu, Trump alisema, “Inaweza kuwa hili au lile.”
Je, hii haimaanishi kuwa Trump anawaweka watawala wa Jordan na Misri katika duara la aibu, hasa kwa vile walishasema awali kwamba hawakukubali uhamishaji huu? Je, hii ina maana kwamba Trump anapanga kuuondoa Ukanda wa Gaza na watu wake ili kuunganisha na umbile la Kiyahudi, hasa kwa kuwa watawala wa Kiarabu, na kwa hakika watawala wote wa Waislamu wamenyamaza kimya mithili ya makaburi bila kusonga mbele kumkabili? Je, hii ina maana kwamba kuna mabadiliko katika sera ya Marekani au ni ile ile lakini kwa mtindo tofauti?
**Jibu:**
Ili kufafanua majibu ya maswali ya hapo juu, tutahakiki mambo yafuatayo:
**1-** Trump hafichi malengo yake, bali anayasema waziwazi, tofauti na mtangulizi wake Biden. Kwa mfano, Biden alikuwa akiwahadaa watu kwamba Marekani inajitahidi kutekeleza mradi wa dola mbili, lakini yalikuwa ni maneno tu yasiyo na maana! Al Jazeera ilichapisha kwenye tovuti yake mnamo tarehe 4/1/2024: “Rais wa Marekani Joe Biden alisema jana, Ijumaa, kwamba kuna miundo kadhaa ya suluhisho la dola mbili, akionyesha kwamba nchi kadhaa katika Umoja wa Mataifa hazina vikosi vyao vya kijeshi...” (Al Jazeera 4/1/2024) yaani, Biden anakusudia serikali ya aina hiyo isiyo na jeshi! Hata hivyo, Trump alitaja ukweli wa lengo lake bila kuwahadaa watu. Alisema wakati wa kampeni yake ya uchaguzi, akisema: “Unapotazama ramani, ramani ya Mashariki ya Kati, ‘Israel’ ni sehemu ndogo ikilinganishwa na ardhi hizi kubwa. Kwa hakika nilisema: ‘Je, kuna njia yoyote ya kupata zaidi?’” (Sky News 19/8/2024), akimaanisha kwamba anataka kupanua umbile la Kiyahudi kwa uhalali wa makaazi katika Ukingo wa Magharibi na kuwapa uhuru wa kunyakua ardhi na kuanzisha makaazi mapya juu yake.
**2-** Hili linathibitishwa na uteuzi wake wa mtu ambaye ana maoni kama yake kama Balozi wa Marekani katika umbile la Kiyahudi, yaani Mike Huckabee, ambaye Trump alimuelezea kwenye akaunti yake ya Ukweli wa Kijamii mnamo tarehe 13/11/2024 kama “Mwenye kuipenda 'Israel' na watu wa 'Israel', na vile vile watu wa 'Israel' wanampenda, na Mike atafanya kazi bila kuchoka kuleta amani Mashariki ya Kati.” Miongoni mwa matamshi ya hapo awali ya Mike Huckabee ni yale ambayo BBC ilichapisha mnamo tarehe 13/11/2024, ikinukuu Chaneli 12 ya Kiyahudi, kwamba Huckabee anajulikana kwa kauli zake za kuunga mkono umbile la Kiyahudi, ikiwa ni pamoja na kauli alizozitoa mwaka 2015 ambapo alisema: “Uhusiano wa kihistoria wa Israel na eneo hilo, uliodumu kwa maelfu ya miaka, uko imara zaidi kuliko uhusiano wa kihistoria wa miaka 400 wa Amerika na Manhattan.” Ana video kwenye mitandao ya kijamii alizochapisha mwaka 2017 ambapo alisema, “Hakuna kitu kama Ukingo wa Magharibi, ni Judea na Samaria, hakuna kitu kama makaazi, ni jamii, ni vitongoji, ni miji, hakuna kitu kama ukaliaji kimabavu.”
**3-** Balozi huyu alirudia kauli zake kwa Chaneli 7 ya Kiyahudi mnamo tarehe 15/11/2024, akisema: “Siwezi kusema kitu ambacho sikiamini. Kamwe sikutaka kutumia neno Ukingo wa Magharibi. Hakuna kitu kama hicho. Ninazungumza juu ya Judea na Samaria. Ninawaambia watu hakuna ukaliaji kimabavu.” Alisema: “Kumbuka kwamba katika kipindi cha miaka minne ambayo Trump alikuwa rais, hakukuwa na rais aliyeiunga mkono Israel zaidi yake katika historia. Kila kitu kuanzia kuitambua Jerusalem kama mji mkuu hadi kuhamisha ubalozi wa Marekani kutoka Tel Aviv hadi Jerusalem na kuitambua Milima ya Golan kama mali halali ya Dola la 'Israel', na pia kutojaribu kuendeleza suluhisho la dola mbili lisiloweza kutekelezeka, kwa sababu halitekelezeki na haliwezi kutekelezwa.” Alisema: “Siamini kwamba suluhisho la dola mbili ni halali. Huu ni msimamo ambao nimeushikilia kwa miaka mingi, na ni msimamo ambao Trump anakubaliana nao, na ninatarajia utaendelea.” Kupitia matamshi haya, vipengele vya sera ya Trump kuhusu kadhia ya Palestina vinadhihirika, ni kuhalalisha uvamizi katika Ukingo wa Magharibi na makaazi ya walowezi.
**4-** Hii ina maana kwamba utawala wa Trump hauna mradi maalum mpya kwa kadhia ya Palestina, kuunda dola kwa ajili yao, bila kujali ukubwa wake. Lakini badala yake mambo yanaelekea kwenye utambuzi rasmi wa Marekani wa umbile la Kiyahudi kupitia uhalali wa makaazi katika Ukingo wa Magharibi, kama inavyoonyeshwa na kauli za balozi wa Marekani katika umbile la Kiyahudi, na kauli yake kwamba Trump anamuunga mkono katika hili. Trump alimsifu, ambapo ina maana kwamba alimsifu kwa mawazo yake kuhusu suala hili. Hii inathibitishwa na Trump kuondoa vikwazo kwa walowezi wa Kiyahudi ambao walifanya ukiukaji ambao Amerika iliona kuwa haramu wakati wa utawala wa Biden. Amani ambayo Trump anamaanisha ni kulikubali umbile la Kiyahudi kwenye ardhi iliyonyakua katika Ukingo wa Magharibi na kujenga makaazi juu yake, huku ikiipa Mamlaka ya Palestina haki ya kubaki na baadhi ya uhuru hivi sasa ili iweze kuendelea kutumikia umbile la Kiyahudi chini ya jina la uratibu wa

***Endelea... UK 7***

usalama, na kuwachosha watu kwa kukusanya ushuru kutoka kwao, kuwalisha watu wa Mamlaka ya Palestina wakitoa baadhi ya huduma za manispaa.

**5-** Trump alijaribu kuonyesha uwezo wake wa kufikia anachotaka na kwamba ana uwezo wa kufanya amani ili kuwahadaa watawala wa eneo hilo na kuwapa matumaini kwani shetani huwapa matumaini wafuasi wake. Al Jazeera iliripoti mnamo tarehe 23/1/2025: "Rais wa Marekani Donald Trump alisema kuwa utawala wake ulifanya mambo mengi zaidi ndani ya siku 4 kuliko utawala wa Rais wa zamani Joe Biden ulivyotimiza katika miaka 4, akisisitiza kwamba kama si utawala wake, makubaliano ya kusitisha mapigano huko Gaza yasingekamilika wiki hii. Pia alitaja kwamba Ufalme wa Saudi Arabia utawekeza dolari bilioni 600 nchini Marekani, lakini ataiomba ifikishe dolari trilioni moja. Walakini, Trump aliambatanisha "mfuko wa zawadi" kwa makubaliano haya kwa umbile la Kiyahudi, kama gazeti la Kiyahudi Yedioth Ahronoth liliripoti mnamo 14/1/2025: "'Israel' itakuwa na haki ya kukomesha usitishaji vita ikiwa itaona ni muhimu, na Ikulu ya White House itatoa uzito wake nyuma ya kufuta vikwazo vilivyowekwa hapo awali na utawala wa Biden kwa baadhi ya walowezi waliotekeleza vitendo vya kihalifu, na itaanzisha kampeni ya kimataifa dhidi ya mahakama mbili za Umoja wa Mataifa zilizoanzisha uchunguzi au mashtaka dhidi ya Israel, hasa dhidi ya Netanyahu na waziri wake wa ulinzi Galant kwa mashtaka ya kufanya uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu."

**6-** Kwa hivyo, Trump, katika muhula wake wa kwanza na wa sasa, ametabanni maslahi ya Kiyahudi, hata maazimio ya kimataifa ambayo yaliwekwa na Marekani na nchi nyingine kubwa, Marekani ilikuwa inazifuata nchi zilizokiuka maazimio hayo. Trump amehujumu maazimio haya yanayopinga maslahi ya Mayahudi. Amehujumu maazimio ya Umoja wa Mataifa ambayo yanauchukulia Ukingo wa Magharibi kuwa ardhi inayokaliwa kwa mabavu ambapo umbile la Kiyahudi halina haki ya kuishi, bali ni lazima liondoke humo hadi kwenye mipaka ya Juni 4, 1967. Pia amehujumu maazimio ya Umoja wa Mataifa kuhusu Jerusalem Mashariki kama ardhi ya Palestina inayokaliwa kwa mabavu, pamoja na maazimio yake kuhusu Milima ya Golan kama ardhi inayokalia kwa mabavu ya Syria, na ametambua uhalali wa uamuzi wa umbile la Kiyahudi kuziunganisha nalo Jerusalem (al-Quds) na Milima ya Golan. Hili linathibitisha kwamba atatambua uhalali wa makaazi hayo na yale ambayo Mayahudi wameyateka hadi sasa katika Ukingo wa Magharibi na kuruhusu makaazi zaidi kuanzishwa au kupanuliwa. Hili limeanza huku akiwasamehe walowezi ambao walikuwa chini ya vikwazo wakati wa muhula wa Biden.

**7-** Trump ataendelea na mpango wake wa kulimakinisha umbile la Kiyahudi kwa kuzifanya nchi zingine katika eneo hilo kuinuka na kuhalalisha mahusiano na umbile hili ili kutambua uhalali wake na unyakuzi wake wa Palestina. Miongoni mwa nchi zilizopendekezwa kwa hili ni Saudi Arabia, haswa kwa vile uhusiano wa Mfalme Mtarajiwa wa Saudia ni mkubwa na Trump, ambaye anafuatilia kwa dhati uhalalishaji mahusiano wa umbile hilo na Saudi Arabia. Hili linaweza lisicheleweshwe, kwani kufuata kikamilifu kwa utawala wa Saudi na kile utawala wa Republican unaoongozwa na Trump unataka kunaeleweka na kila mtu mwenye macho na ufahamu. Trump alitangaza mnamo tarehe 23/1/2025 kwamba "Saudi Arabia itawekeza dolari bilioni 600 katika uchumi wa Marekani, na nitaomba kuongeza hadi dolari trilioni." (Al-Hurra America, 23/1/2025), na alisema kwamba hili lilifanyika kupitia maongezi ya simu na Mfalme Mtarajiwa wa Saudia, Bin Salman, jioni ya Jumatano 22/1/2025. Yaani, kwa simu moja tu, mtawala mkuu wa Saudi Arabia mara moja alitii ombi la rais wa Amerika la kuunga mkono uchumi wa Amerika kwa mamia ya mabilioni ya dolari. Hii inaonyesha kiwango cha utayari wa serikali ya Saudi kutii maombi ya Amerika wakati wa muhula wa Trump. Kwa hiyo, kwa simu nyingine tu, Bin Salman atatangaza utayarifu wake wa kuhalalisha mahusiano na umbile la Kiyahudi atakapotakiwa kufanya hivyo.

**8-** Kwa hiyo, yeyote anayetafakari hatua za Trump katika kuunga mkono umbile la Kiyahudi atapata kauli ya Trump imejumuishwa katika swali kuhusu kuondoa Ukanda wa Gaza kutokana na watu wake na kuuunganisha kwa Mayahudi, hasa alipoulizwa ikiwa hili lilikuwa pendekezo la muda mfupi au la muda mrefu, Trump alisema, "Inaweza kuwa hili au lile" (Al Jazeera 26/1/202), yeyote anayetafakari hili ataliona kuwa ni jambo la kawaida kwa Trump. Ama kuhusu yale yaliyosemwa katika swali: "Je, hii haimaanishi kwamba Trump anawaweka watawala wa Jordan na Misri katika duara la aibu, hasa kwa vile walishatangulia kusema kwamba hawakukubali uhamishaji huu?" Trump hajali kuhusu wao, iwe wanakosa hewa au la, haswa kwa vile hapo awali alitoa kauli iliyo wazi zaidi kuliko kauli hii, hapo awali alisema: "Unapoangalia ramani, ramani ya Mashariki ya Kati, 'Israel' ni sehemu ndogo sana ikilinganishwa na ardhi hizi kubwa. Kwa kweli niliuliza: 'Je, kuna njia yoyote ya kupata zaidi?'" (Sky News 19/8/2024). Kauli yake ya awali ilikuwa juu ya kupanua umbile, na kauli yake ya sasa ni kauli ya mojawapo ya njia za kupanua umbile hilo, na inaonekana kwamba Trump anataka kuandaa mazingira kwa ajili ya watawala vibaraka kuendelea na uhamishaji huu wa lazima ambao watawala walikuwa wameukataa hapo awali, hasa nchini Misri na Jordan. Kwa maana nyengine, ni mchakato wa "kuyajaribu maji" ili kuona kama watawala hawa wanaweza kuwashinikiza watu kutekeleza kauli ya Trump na kuwaondoa katika nchi zao, kuwaondoa katika nchi zao, kuwaunganisha na Mayahudi, au kuakhirisha hili hadi wakati mwingine ambao Trump ataona kuwa unafaa ikiwa watu watasimama dhidi ya tawala mbili na kuwazuia na hatua hii, ambayo ni khiyana kwa Mwenyezi Mungu, Mtume wake na waumini.

**9-** Tunatambua kwamba watawala katika nchi za Kiislamu, hasa zinazoizunguka Palestina, hawaoni haya mbele ya Mwenyezi Mungu, Mtume wake, na waumini, na kutekeleza amri ya Trump ni moja ya vipaumbele vyao. Hili liko wazi kutokana na harakati zao za kumpongeza Trump kwa ushindi wake katika uchaguzi

***Endelea... UK 8***

na urais wake wa Marekani, ingawa hakuficha uaminifu wake kwa Mayahudi na uadui wake kwa Uislamu na Waislamu. Walakini, watawala hawa walishindana kumpongeza:

**a-** RT - Arab World News - 6/11/2024, ilichapishwa: Ikinukuu shirika la habari la Saudi SPA, pongezi za mfalme wa Saudi kwa Trump ambaye alisifu “uhusiano tofauti wa karibu wa kihistoria kati ya nchi hizo mbili marafiki na watu, ambao kila mtu anataka kuimarisha na kuendeleza katika nyanja zote.” Pia ilichapisha pongezi za rais wa Uturuki kupitia jukwaa la X: “Ninampongeza rafiki yangu Donald Trump ambaye alishinda uchaguzi wa rais…tunatumai kuwa uhusiano wa Uturuki na Marekani utaimarishwa.”

**b-** Al Jazeera ilichapisha mnamo tarehe 6/11/2024 pongezi za Rais wa Misri: “Ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Rais Mteule wa Marekani Donald J. Trump ... na kukuza ushirikiano wa kimkakati kati ya Misri na Marekani na watu wao… kuendeleza maslahi ya pamoja ya nchi hizo mbili marafiki.” Na kutoka kwa Mfalme wa Jordan, “Pongezi za dhati kwa Rais Donald Trump kwa kushinda uchaguzi wa urais wa Marekani.” Ninatarajia kufanya kazi nanyi tena ili kuimarisha ushirikiano wa muda mrefu wa Jordan na Marekani...” Pia kutoka kwa Waziri Mkuu wa Pakistan kwenye tovuti ya X, “Hongera kwa Rais Mteule Donald Trump kwa ushindi wake wa kihistoria kwa muhula wa pili.”

**c-** Hata Ahmad al-Sharaa, mkuu wa utawala mpya nchini Syria, alifuata njia hiyo hiyo na akachapisha kwenye Facebook mnamo tarehe 20/1/2025: “Kwa niaba ya uongozi na watu wa Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, nampongeza Donald Trump kama Rais wa Marekani.” Alisema, “Tuna imani kuwa yeye ndiye kiongozi wa kuleta amani Mashariki ya Kati na kuregesha utulivu katika eneo hili.”

Hawa ndio watawala wa nchi za Waislamu. Mwenyezi Mungu awalaani wamedanganya kiasi gani.

**10-** Hata hivyo, tunatambua pia kwamba Umma wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) pamoja na watu wake waaminifu na wanyoofu, utazifanya kauli za Trump na wafuasi wake kutoka kwa watawala hao, kuwa vumbi lililotawanyika. Kushikamana kwa watu wa Palestina, ardhi iliyobarikiwa, ni jambo linalojulikana sana katika nchi yao. Yeyote aliyewatazama wakitembea kwa maelfu kwa miguu yao, katika hali ngumu ya hewa na hata hali ngumu zaidi ya ardhini, wakiharakisha kwenda kwenye nyumba zao, ambazo wanajua zimevunjwa na uvamizi wa kikatili wa Mayahudi, lakini kwao wanachukulia kuzifikia kuwa ni ushindi mkubwa. Yeyote aliyeyaona yote hayo na kuyatafakari anatambua kwamba kauli za Trump na njama zake za kuiondoa Palestina watu wake, hata kama zitachanganywa na njama za watiifu wake kutoka kwa watawala wa Ruwaibidha (wajinga wazembe), yote hayo yatawarudia wao:

﴿وَقَدْ مَكَرُوا مَكْرَهُمْ وَعِنْدَ اللهِ مَكْرُهُمْ وَإِنْ كَانَ مَكْرُهُمْ لِتَزُولَ مِنْهُ الْجِبَالُ﴾

“Na kwa hakika walifanya vitimbi vyao, na vitimbi vyao anavijua Mwenyezi Mungu. Wala vitimbi vyao si vya kuondosha milima.” [Ibrahim: 46].

Kisha Ardhi iliyobarikiwa itaregea kwa watu wake, nyumba ya Uislamu. Watawala wote hawa Ruwaibidha watatoweka, na dola ya Kiislamu, Khilafah Rashida, itaregea, Mwenyezi Mungu akipenda. Kupigana na Mayahudi na kuondoa uvamizi wao kutatokea, Mwenyezi Mungu akipenda. Amesema Sadiq al-Musadaq (Mkweli, Mwaminifu) (saw) katika Musnad ya Ahmad kutoka kwa Hudhayfah:

« ...ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ »

“Kisha itakuweko Khilafah kwa Njia ya Utume” Al-Bukhari pia amepokea kutoka kwa Abdullah bin Omar, Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote wawili, ambaye amesema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema:

«...تُقَاتِلُكُمْ الْيَهُودُ فَتُسَلَّطُونَ عَلَيْهِمْ»

“Mayahudi watapigana nanyi na nyinyi mtawashinda” Muslim pia ameipokewa kwa maneno ya Ibn Umar, kutoka kwa Mtume (saw) ambaye amesema:

«...لَتُقَاتِلُنَّ الْيَهُودَ فَلَتَقْتُلُنَّهُمْ»

“Mtapigana na Mayahudi na mtawauwa...” Kisha ardhi itang’aa kwa ushindi wa Mwenyezi Mungu, Al-Qawi Al-Aziz.

**11-** Lakini kama tulivyotangulia kusema, na tunarudia katika hitimisho hili:

“Hata hivyo, sheria ya Mwenyezi Mungu ilitaka asiteremshe Malaika kutoka mbinguni ili watusimamishie Khilafah kupigana na adui yetu huku sisi tukiwa tumekaa.

Bali, Yeye huwateremsha Malaika Wake kuwa ni wenye kutilia nguvu na kutoa bishara njema ya Nusrah (ushindi) kwa watu wanaomuamini Mola wao Mlezi, na akawazidishia uwongofu, wanajeshi wa Kiislamu, wenye subira katika vita, wanaolindwa na kiongozi wao na wanaopigana na maadui zao nyuma yake:

﴿بَلَى إِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا وَيَأْتُوكُمْ مِنْ فَوْرِهِمْ هَذَا يُمْدِدْكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ آلَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُسَوِّمِينَ﴾

“Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamngu na hata maadui wakikutokeeni kwa ghafla, basi hapo Mola wenu Mlezi atakusaidieni kwa Malaika elfu tano wanao shambulia kwa nguvu.” [Aali-Imran: 125]. Hapo tutakuwa miongoni mwa wanaostahiki bishara njema:

﴿نَصْرٌ مِنَ اللهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ﴾

“… Nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi ulio karibu! Na wabashirieni Waumini!” [As-Saf: 13].”

**28 Rajab 1446 H**

**28/1/2025 M**